



THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

SCHOOL BASED ASSESSMENT

KISWAHILI

SEHEMU A

Zoezi 1 na 2

Gredi ya 4-2026

NAKALA YA MWALIMU

Muda: Dakika 15 kwa kila mwanafunzi

Sehemu A inatathmini Stadi ya Kusikiliza na Kuzungumza. Inajumuisha mazoezi matatu:

- i. Mazungumzo ya ana kwa ana
- ii. Ufahamu wa Kusikiliza
- iii. Kusoma kwa sauti

Maagizo ya jumla

1. Wafahamishe **wanafunzi wote** kwamba mazoezi yote katika sehemu hii yatakuwa tathmini ya ana kwa ana. Kila mwanafunzi atakuwa na zamu yake ya kutathminiwa; mmoja baada ya mwingine.
2. Wafahamishe wanafunzi wote kwamba karatasi hii ina mazoezi matatu:
 - i. **Mazungumzo ya ana kwa ana**
 - ii. **Ufahamu wa Kusikiliza**
 - iii. **Kusoma kwa Sauti**
3. Mwandalie mwanafunzi kiti au dawati kutazamana nawe.
4. Tanguliza kila zoezi na umfahamishe mwanafunzi matarajio ya kila zoezi.
5. Mfahamishe mwanafunzi kukamilika kwa kila zoezi.
6. Tathmini umilisi wa mwanafunzi kwa mujibu wa mwongozo wa kutathminia. Weka rekodi ya matokeo ya tathmini.

ZOEZI 1A: MAZUNGUMZO YA ANA KWA ANA

Maagizo maalum

- i. Andaa mazingira mazuri ya tathmini kwa kumkaribisha mwanafunzi.
- ii. Mwamkue na kumwomba akae.
- iii. Jitambulisha kwake kwa kusema, 'Mimi ni mwalimu _____'.
- iv. Muulize jina lake.
- v. Anza tathmini kwa kusema,

“Leo ningependa tuzungumze kuhusu nidhamu wakati wa kula.”

1. Watu wanapokula huketi mahali maalum. Je, nyinyi huketi wapi wakati mnakula mkiwa nyumbani au shuleni?
(Mwanafunzi ajibu)
2. Wakati wa kula, ni vyema kuketi badala ya kusimama. Nitajie jambo lingine ambalo unapaswa kufanya wakati wa kula ili kuonyesha nidhamu.
(Mwanafunzi ajibu)
3. Je, unapokula harakaharaka, unafikiri unaweza kupata hasara gani?
(Mwanafunzi ajibu)
4. Watu wanapokula, ni vyema wawe na **nidhamu**. Neno **nidhamu** lina maana gani?
(Mwanafunzi ajibu)

ZOEZI 1B: UFAHAMU WA KUSIKILIZA

Maagizo maalum

- i. Msomee mwanafunzi kifungu kifuatacho **mara mbili**.
- ii. Mjulishe kuwa atajibu maswali baada ya kusomewa kifungu mara ya pili.

Sara ni mmoja wa wanaskauti shuleni mwetu. Yeye ndiye mwenye umri mdogo zaidi katika kikundi hicho. Ijumaa iliyopita, ilikuwa zamu yake kupandisha bendera ya taifa.

Sote tulisimama wima tukisubiri maagizo ili tuimbe wimbo wa taifa na wimbo wa Afrika Mashariki ambazo tunazipenda sana. Sara na wenzake wawili walielekea kwenye mlingoti na kusimama. Firimbi ilipulizwa. Sara alipiga hatua mbele na kuivuta kamba ya bendera ya nchi yetu akaanza kuipandisha. Baada ya kuipandisha, bendera ilianza kupeperushwa huku na kule na upepo wa asubuhi.

Sara alirudi nyuma hatua mbili. Alipiga saluti na kujiunga nasi ili kuimba wimbo wa taifa na wimbo wa Afrika Mashariki. Wakati huo wote, tulikuwa tumeikodolea macho bendera yetu kule juu. Tulikuwa tukifikiria kuhusu rangi za bendera yetu. Nyeusi ilitukumbusha ngozi yetu. Rangi ya kijani ilitukumbusha ardhi yetu yenye rutuba nayo nyeupe iliashiria amani. Rangi nyekundu ilitukumbusha damu iliyomwagika wakati wa kupigania uhuru. Shule nzima ilimpigia Sara makofi.

5. Sara alipandisha bendera siku gani?
(Mwanafunzi ajibu)
6. Wanafunzi wa shule ya kina Sara wanaipenda nchi yao kwani _____
(Mwanafunzi ajibu)
7. Je, unafikiri wanafunzi wengine walifanya nini baada ya kuona uhodari wa Sara?
(Mwanafunzi ajibu)
8. Ilikuwa zamu ya Sara kupandisha bendera ya taifa. Neno **zamu** lina maana gani?
(Mwanafunzi ajibu)

ZOEZI 2 : KUSOMA KWA SAUTI

Maagizo maalum

- i. Mfahamishe mwanafunzi matarajio ya Zoezi la Kusoma. (Zingatia mwongozo wa kutathminia Kusoma kwa sauti).
- ii. Mpe mwanafunzi nakala atakayoisoma kwa sauti.
- iii. Mwanafunzi anaposoma, sikiliza na kurekodi idadi ya maneno anayosoma kwa muda wa **dakika moja**.
- iv. Onyesha kwa mshazari (/) mahali mwanafunzi alipofikia kusoma **dakika moja** ikikamilika.
- v. Mruhusu mwanafunzi kusoma mpaka mwisho wa kifungu.
- vi. Pigia mstari maneno **yote** ambayo mwanafunzi atashindwa kuyasoma au kuyatamka vizuri.

vii. *Rekodi idadi ya maneno ambayo mwanafunzi ameweza **kusoma kwa usahihi** kwa dakika moja. (Baada ya kuondoa yaliyotamkwa vibaya au/na aliyoshindwa kutamka)*

viii. *Rekodi viwango vya umilisi wa mwanafunzi kwa kuzingatia mwongozo uliopewa.*

ix. *Hakikisha una nakala ya kurekodia tathmini hii. (Iwe na majina ya wanafunzi wote.)*

x. *Ukiwa tayari kuanza tathmini, sema,*

“Sasa naomba unisomee kifungu hiki kwa sauti.”

Tembo na Tumbili waliishi katika msitu wa Dunda. Tembo alifanya ¹⁰ biashara ya kuuza matunda. Matunda hayo aliyapata kutokana na bidii ²⁰ yake shambani. Faida aliyopata aliitumia vyema. Alinunua shamba kubwa ili ³⁰ apanue kilimo cha matunda. Baada ya miaka michache, Tembo alikuwa ⁴⁰ tajiri. Alianzisha biashara nyingine ya magari ya usafiri. Alikuwa na ⁵⁰ mabasi kumi. Mabasi hayo pia yalimletea faida kubwa. Wanyama wengi ⁶⁰ walimtaka awashauri kuhusu biashara na matumizi ya pesa.

Tumbili naye ⁷⁰ aliuza hanchifu, njugu na pipi//. Faida aliyopata aliitumia vibaya. Alinunua vitu vya anasa visivyo muhimu kwa maisha yake. Punde si punde, alianza kuomba pesa kwa Tembo. Ingawa Tembo alimsaidia, alimshauri abadilishe mwenendo wake mbaya.